Guilford County Schools

# 2017-18
# MPANGO WA HALI MBAYA YA HEWA

**Shule za Kata ya Guilford (GCS) huamua aje, ikiwa watafunga au kuchelewesha shule wakati hali mbaya ya hewa imetabiriwa?**

**Msimamizi** amempa **Afisa Mkuu wa Shughuli** wajibu wa kupendekeza kufungwa au kuchelewesha shule au kuwachilia wanafunzi mapema, iwapo hali mbaya ya hewa itatabiriwa. **Afisa Mkuu wa Shughuli** husimamia **Mkurugenzi wa Usafir**i na timu ya **Wasimamizi wa Usafiri** ambao wamepewa kazi ya kutathmini barabara na hali ya hewa katika Kata ya Guilford.

Ikiwa hali mbaya ya hewa iliyotabiriwa inatishia usalama wa basi ya shule barabarani, **Wasimamizi wa Usafiri** hukagua baraba zilizoteuliwa na kushauri **Mkurugenzi wa Usafiri** kuhusu hali ya barabara kabla ya saa kumi na moja asubuhi. Mkurugenzi huzingatia taarifa zote zilizotolewa na wasimamizi kuhusu hali za barabara, anatathmini picha za rada, anashauriana na tawi la mitaa la Huduma ya Taifa ya Hali ya hewa, na kutoa mojawapo ya mapendekezo yafuatayo kwa **Afisa Mkuu wa Shughuli**:

1. Shule inafungua wakati wa kawaida;
2. Kufunguliwa kwa shule kutachelewa kwa saa moja au masaa mawili;
3. Shule itafungwa mapema; au,
4. Shule haitafunguliwa siku hiyo.

**Afisa Mkuu wa Shughuli** hushauriana na **Msimamizi,** ambaye hufanya uamuzi wa mwisho. Uamuzi wa kufunga au kuchelewesha shule, ikiwa ni pamoja na muda gani wa kuchelewesha, utatangazwa na **Mkurugenzi wa Mawasiliano** katika vyombo vya habari, kupitia Connect-Ed ®, kuchapishwa kwenye tovuti ya GCS (www.gcsnc.com) na kwenye GCSTV 2 kabla ya saa kumi na moja na nusu asubuhi. *Kama shule zinafungua kwa wakati wa kawaida, tangazo halitatolewa.Kwa hivyo, hakuna matangazo yatakuwa kwenye vyombo vya habari kuonyesha kwamba shule itafanya kazi katika ratiba ya kawaida*. Kama hali ya hewa itabadilika baada ya siku ya shule kuanza, uamuzi kuhusu kuachiliwa mapema utafanywa haraka iwezekanavyo.

Wakati wowote iwezekanavyo, kama uamuzi kuhusu kufungwa kwa shule unaweza kufanywa jioni kabla, **Afisa Mkuu wa Shughuli** atafahamisha **Msimamizi Mkuu** kuhusu mapendekezo na kupata kibali cha mwisho kabla ya saa kumi na nusu jioni.

Ikiwa shule zitafunga kwa siku moja, hali za barabara zitatathminiwa upya mchana huo na maoni kutolewa katika vyombo vya habari wakati wa habari za jioni, wakati wowote iwezekanavyo. Ikiwa hali ya barabara haina uwezekano wa kubadilika kabla ya asubuhi iliyofuata, shule itasitishwa.

Arifa itatangazwa kwenye vyombo vya habari, kuchapishwa kwenye tovuti ya GCS (www.gcsnc.com) na kutangazwa kwenye GCSTV 2. Mfumo wa Connect ® na vyombo vya habari vya kijamii pia vitatumiwa kutangaza. Ikiwezekana, tangazo litatolewa kwenye taarifa ya saa kumi na mbili jioni.

Ikiwa tathmini ya mchana itaonyesha kwamba kuna uwezekano wa shule kufunguliwa siku inayofuata, uamuzi huo unaweza kuairishwa hadi asubuhi iliyofuata na tangazo litatolewa kabla ya saa kumi na moja asubuhi.

**Kuongeza Muda wa Kusitishwa kwa Shule Kutokana na Hali Mbaya ya Hewa:**

Mwishoni mwa siku ya **tano** ya shule, ikiwa baadhi ya barabara zinabakia kuwa hatari kwa usafiri wa basi ya shule na haziwezi kuwa salama ndani ya siku tatu zifuatazo, **Dereva wa Basi** au **Wasimamizi wa Usafiri** watapiga simu kwa wazazi / walezi wa wanafunzi ambao wamewapa nambari (angalia hapa chini) na ambao wanaishi kwenye maeneo ya barabara zisizopitika. Dereva atawapa kituo cha basi kilicho karibu na kilichopendekezwa/na masaa wanakayokuwa kwenye barabara hiyo. Mzazi / mlezi anahitaji kumshauri dereva wa basi au msimamizi wa usafiri ikiwa atamleta au hawezi kumleta mwanafunzi kwenye kituo cha basi kilichopendekezwa ili aweze kuchukua basi. Kwa madhumuni ya kupanga, na kuepuka kuchanganyikiwa, mtoto huyo atarudishwa kwenye kituo hicho cha basi mchana huo. Wakati wa kushuka kutoka kwa basi, dereva atampa mwanafunzi maelezo kwa wazazi na / au walezi kuhusu sehemu kituo cha basi kitakuwa asubuhi itakayo fuata.

*Ikiwa mwanafunzi anachukuliwa au kurudishwa kwenye kituo cha huduma ya watoto, ni wajibu wa mzazi / mlezi kushauri kituo cha huduma ya watoto kukumbatia mpango huu na kukutana na basi katika mahali mbadala.*

Madereva wa mabasi wameagizwa kukusanya nambari za simu za nyumbani za wanafunzi wote kutoka fomu ya kawaida ya Shule za Kata ya Guilford ambayo imesainiwa na mkurugenzi wa usafiri. Wazazi / walezi wanaulizwa kukamilisha fomu hiyo na kurudisha moja kwa moja kwa dereva wa basi. Madereva wa mabasi wa wanafunzi wenye mahitaji maalum tayari wana namba za simu za nyumbani lakini wazazi wa wanafunzi hawa watatakiwa kuthibitisha namba hizo na dereva wakati wa kuchukua au kuleta mwanafunzi.

## Shughuli za Ziada za Shule

**Shule za Upili** - Siku ya kwanza ya shule kufungwa kutokana na hali mbaya ya hewa, shughuli zote za shule zitasitishwa, isipokuwa ruhusa iwe imetolewa na **Mkuu wa Shule**. Hakuna wanafunzi anapaswa kuadhibiwa kwa kushindwa kuhudhuria shughuli wakati shule imefungwa, hata kama idhini ya imetolewa.

**Shule za Msingi na za Kati** - Hakuna shughuli za shule zitafanyika wakati shule imefungwa au imeachiliwa mapema kutokana na hali mbaya ya hewa, ikiwa ni pamoja na programu ya ACES, michezo, mazoezi, maonyesho, nk, isipokuwa idhini ya kuendelea iwe imetolewa na **Mkuu wa Shule.**

Hali mbaya ya hewa inaweza pia kusababisha shughuli za ziada za shule kusitishwa hata wakati siku za shule zinafungwa wakati wa kawaida. Kufungwa kutokana na hali hii kutatangazwa na shule, kutangaza katika GCSTV 2 na kuchapishwa mtandaoni kwenye www.gcsnc.com.

## Hali Kali ya hewa - Ufuatiliaji na Tahadhari

**Ufuatiliaji wa hali kali ya hewa** - Shughuli za usafiri zitaendelea kama kawaida wakati wa ufuatiliaji wa hali kali ya hewa. **Mkurugenzi wa Usafiri** huchunguza hali ili kuhakikisha mabasi ya shule yanaweza kusafiri kwa usalama. Ili kudumisha uthabiti kwenye ratiba, mabasi ya shule hayatatoka kwenye barabara za kawaida zilizopangwa na hakutakuwa na vituo vya ziada vya mabasi.

**Onyo la hali kali ya hewa -** Ikiwa onyo la hali kali ya hewa litatolewa kabla ya mabasi kuchukua wanafunzi na yakiwa mbali na chuo, shughuli za basi zitasimamishwa, na wanafunzi chini ya uongozi wa wakuu wao, watajikinga katika jengo la shule hadi mwisho wa onyo. Ikiwa onyo la hali kali ya hewa litatolewa baada ya mabasi kuondoka kutoka shuleni, madereva wa mabasi wataulizwa kuendelea kwa uangalifu hadi kwenye eneo la usalama na kusimamisha mabasi mpaka mwisho wa onyo la dhoruba.